
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA | **WIZARA YA KATIBA NA SHERIA**

ZIARA MAALUM YA WAZIRI KABUDI MKOANI

# MBEYA



## SHERIA BULLETIN

Toleo la 16

> **Rais Samia kanituma kukagua, kuzindua miradi ya maendeleo na kuwasikiliza nyie wananchi wa Mbeya.**
>
> —Mhe. Prof. P.A.J.M Kabudi—





*Jarida Maalum*


**ELIAKIM C. MASWI**
Katibu Mkuu

**LUSAJO MWAKABUKU**
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

**WAJUMBE**
William Mabusi | Hyasinta Kissima | Castus Busolo
**Msanifu Kurasa:** Lusajo Mwakabuku

# Waziri Kabudi aagiza bweni kukamilika kabla ya kufika Januari.



*Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Prof. Palamagamba John Kabudi akikagua eneo la vyoo katika bweni hilo jipya ujenzi unaotarajiwa kugharimu zaidi ya shilingi milioni Mia Moja na Hamsini, bweni la wanafunzi wa kike wenye mahitaji maalumu wa Shule ya Msingi Sama.*

Na Lusajo Mwakabuku & Nebart Msokwa

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Prof. Palamagamba John Kabudi ameagiza Halmashauri ya Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya kukamilisha haraka ujenzi wa Bweni la wanafunzi wa kike wenye mahitaji maalumu wa Shule ya Msingi Sama ili kuwapunguzia kero ya kusafiri umbali mrefu kwenda shuleni.

Prof. Kabudi ametoa agizo hilo alipoweka jiwe la msingi la ujenzi wa bweni hilo ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake ya kukagua utekelezaji wa miradi, kuzindua na kuweka mawe ya msingi kwenye ujenzi wa miradi mbalimbali mkoani Mbeya.

Jengo hilo linajengwa kwa gharama ya zaidi ya Sh. Milioni 100 ambapo alisema jengo hilo linatakiwa likamilike kabla ya mwezi januari ili wanafunzi hao waendelee kulitumia.

Amesema lengo la serikali ni kuboresha mazingira ya upatikanaji wa elimu kwa wanafunzi wote bila kujali hali zao huku akisisitiza kuwa elimu ni haki ya kila mtoto kwa mujibu wa sheria za nchi.

"Nimeambiwa bado Sh. Milioni 30 kwa ajili ya kukamilisha jengo hili, mkurugenzi hakikisha unaleta fedha hizo haraka ili jengo likamilike, mwezi januari jengo lianze kutumika, hakuna kisingizio hapa," amesema Prof. Kabudi.

Aidha baada ya kauli hiyo ya Waziri Kabudi, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kyela aliahidi kutimiza hilo na ikatolewa ahadi kwamba hadi kufika mwezi wa Kumi na Mbili mwaka huu jengo litakamilika tayari kwa kuanza kutumika Januari.

Amesema Serikali imetoa fedha nyingi kwa ajili ya uboreshaji wa sekta ya elimu na hivyo akawataka viongozi wa serikali kuhakikisha wanasimamia fedha hizo ili zilete matokeo Chanya.

**"Nimeambiwa bado Sh. Milioni 30 kwa ajili ya kukamilisha jengo hili, mkurugenzi hakikisha unaleta fedha hizo haraka ili jengo likamilike, mwezi januari jengo lianze kutumika, hakuna kisingizio hapa," amesema Prof. Kabudi.**



*Waziri wa Katiba na Sheria, Prof. Palamagamba John Kabudi akimwagilia mti alioupanda mara baada ya kuzindua bweni hilo la wanafunzi wa kike wenye mahitaji maalum.*

# BARABARA YA LWANGWA GESI KUINUA UCHUMI WA WANANCHI BUSOKELO

Na Lusajo Mwakabuku & Lennox Kisila

Waziri wa Katiba na Sheria Prof. Palamagamba John Kabudi ametembelea na kukagua mradi wa barabara ya Lwangwa-Kyejo inayojengwa kwa kiwango cha lami, iliyogharimu shilingi billion 6.1. kwa lengo la kuinua uchumi wa wananchi hususan wakulima ili waweza kusafirisha mazao yao kwa urahisi.

Akizungumza na wananchi wa halmashauri ya wilaya ya busokelo katika eneo la soko la Ntangasale Lwangwa Mjini, Prof. Kabudi amesema kukamilika kwa barabara hiyo kutarahisisha huduma ya usafirishaji kwa wananchi kutoka mazao yao kupeleka sokoni sambamba na kusambaza bidhaa na malighafi mbalimbali.

Kwa upande wake mkurugenzi mtendaji wa halmashauri ya Busokelo Bi, Loema Peter amesema baada ya Barabara hiyo kukamilika itainua uchumi wa mtu mmoja mmoja na ukusasanji wa mapato utaongezeka kwani kwa kipindi kirefu wanachi walishindwa kupeleka mazao yao sokoni kutona na ubovu wa barabara hiyo kutoka mashambani na kwamba wananchi wamefarika sana na hatua hii ya Rais Samia kuwakumbuka wanachi wa Busokelo.

Aidha naye mbunge wa jimbo la Busokelo Mh,Atupele fredy Mwakibete ameishukuru serikali ya awamu ya sita kwa kutoa fedha nyingi kwaajili ya miradi mbalimbali ikiwa ya Elimu,afya na maji kwani wananchi wanaedelea kupata matunda ya serikali yao. Hata hivyo Mwakibete amemuomba waziri kujenga soko kubwa katika eneo la Ntangasale kwani wajasiriamali hasa wakina mama wanashindwa kufanya biashara zao kwa uhuru kutokana na miundumbinu ya soko kutokuwa rafiki.

Akitoa majibu kwa baadhi ya hoja mbalimbali zilizoibuliwa, Waziri Kabudi amesema suala la ujenzi wa soko litafanyiwa kazi kwani ni maagizo rasmi kutoka kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha yanawekwa mazingira rafiki kwa wananchi katika maeneo wanayofanyia shughuli zao zinazowaingizia kipato.

Hii ni ziara maalum ambayo Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Prof. Palamagamba John Kabudi yupo Mkoani Mbeya kukagua miradi ya maendeleo, kuweka maziwe ya msingi pamoja na kuzungumza na wananchi katika mikutano ya hadhara katika Halmashauri zote mkoani humo.




*Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Prof. Palamagamba John Kabudiakiambatana na Mkuu wa Wilaya ya Rungwe Mhe. Jaffar Haniu wakati wakikagua ujenzi wa barabara ya Lwangwa-Kyejo inayojengwa kwa kiwango cha lami*




## USAJILI WA MASHIRIKA YANAYOTOA MSAADA WA KISHERIA

Tembelea Tovuti ya Wizara ya Katiba na Sheria ya *www.sheria.go.tz*, kisha bonyeza eneo la Huduma Mtandao, kisha chagua Usajili wa watoa huduma za Msaada wa Kisheria.

Au ingia moja kwa moja kwenye anuani ya *https://legalaid.sheria.go.tz;* naNenda sehemu iliyoandikwa **REGISTRATION** kisha tengeneza akaunti ya Shirika kisha fuata maelekezo kusajili Shirika.



## NISHATI

### Kuhusu Sekta ya Nishati

Waziri Kabudi Amesema Wananchi wa Rungwe wajiandae kupata Umeme wa Kutosha zaidi hasa kupitia Ujenzi wa Mradi wa kufua Umeme kupitia Mlima Mbozi utakaozalisha Umeme kiasi cha Megawati 30 na kutoka Kiejo Megawati 10.



## UCHAGUZI

### Na kuhusu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa

Waziri Kabudi amewaomba Wananchi Kuchagua Viongozi wanaosikiliza kero zao na kuzipeleka mahala panapohusika na si kuchagua viongozi mizigo ambao hawawezi kuwawakilisha Vyema katika mahitaji yao. Aidha Kabudi akasisitiza kuwa utekelezaji wa kazi za wananchi unaanzia ngazi za chini hivyo ni muhimu kushiriki katika

## NENO LA RC

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya Komredi Juma Z. Homera amewataka wananchi kuiunga mkono Serikali hasa katika mapambano ya kuhakikisha jamii yote ya wanarungwe inapata mahitaji ya Msingi kwa kutunza na kuilinda miradi ya kimaendeleo ambayo ni maono na Dhamira ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt: Samia Suluhu Hassan ya kuwatumikia wananchi.



# Dkt. Samia anasimamia siasa za maendeleo - Kabudi

Na Lusajo Mwakabuku

*"Rais Samia anafanya kazi kubwa sana, ushahidi mkubwa ni huu hapa mnaojionea wenyewe, na pia maendeleo mnayoyaona hapa kwenye jimbo lenu la Rungwe ndio maendeleo yanayofanyika kila eneo katika nchi yetu"* ***Prof. Kabudi***

Waziri Wa Katiba na Sheria Mh. Prof. Palamagamba John Kabudi Amesema Dkt: Samia Suluhu Hassan amemtuma kuwaambia Wananchi wa Wilaya ya Rungwe kuwa yeye anafanya Siasa ya Maendeleo na si za vurugu wala mitafaruku zaidi amewekeza kwenye maendeleo hususan kwa wananchi wa Vijijini.

Kabudi ameyasema hayo wakati akizungumza na Wananchi wa Wilaya ya Rungwe wakati ikiwa ni sehemu ya ziara yake ya Kukagua Ujenzi wa Stendi ya Mabasi Madogo ambayo imegharimu kiasi cha shilingi Milioni 380 kutoka Mfuko wa Mapato ya Ndani ya Halmashauri.

"Labda Niwambie Vijana Maendeleo tunayoyaona Leo hapa wengine hatukuyatarajia, Leo Maji yapo, Vituo vya Afya vimejengwa, Madarasa yanajengwa ya kutosha, Mawasiliano yameimarishwa kupitia Ujenzi wa Minara ya Simu, Barabara zinaendelea kujengwa" Alisema Prof. Kabudi.



*Mkuu wa Mkoa wa Mbeya Komredi Juma Z. Homera na Mkuu wa Wilaya ya Rungwe Bwn Jaffar Haniu wakibadilishana mawazo.*



*Mradi wa barabara ya Lwangwa-Kyejo inayojengwa kwa kiwango cha lami, iliyogharimu shilingi billion 6.1 ikikaguliwa.*



*Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Palamagamba John Kabudi akiongea na wananchi wa Tukuyu - Rungwe.*



Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Palamagamba John Kabudi akikagua shamba la michikichi ambapo serikali imetoa ruzuku ya miche ya kisasa ya michikichi kwa lengo la kuhamasisha zao hilo.

# “Mzihifadhi mbegu za asili zampunga” - Kabudi

Na Lusajo Mwakabuku

SERIKALI imeagiza wataalamu wa kilimo katika Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya, kuhifadhi mbegu za asili za mpunga ambao umeipatia wilaya hiyo sifa katika masoko ya ndani na nje ya nchi kutokana na ubora wake ili isitoweke na iendelee kuwanufaisha wananchi.

Waziri wa Katiba na Sheria, Prof. Palamagamba Kabudi alitoa agizo hilo kwenye mkutano wa hadhara na wananchi wa Wilaya ya Kyela ikiwa ni sehemu ya mwendelezo wa ziara ya kikazi ya kutembelea halmashauri zote za mkoa huo.

Alisema mchele kutoka katika Wilaya hiyo umekuwa ukitumika katika hoteli za kimataifa kutokana na ubora wake pamoja na harufu nzuri na kwamba umekuwa ukiwaingizia wakulima fedha nyingi.

Alisema katika miaka ya karibuni aina hiyo yam punga umeanza kupotea kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ongezeko la magugu na hivyo kuwalazimu wakulima kuanza kupanda aina zingine za mpunga ambao ubora wake ni mdogo.

“Naomba aina hiyo ya mpunga muitunze ili isipotee kabisa, lakini pia nawaomba wakulima muendelee kulima aina hii kwa sababu ina soko zuri sana nje ya nchi, ndio aina ya mchele ambao unatumika kwenye hoteli za nyota tano duniani,” alisema Prof. Kabudi.

Aidha alisema mbali na aina hiyo ya mpunga pia wilaya ya Kyela ndiyo inayoongoza duniani kwa kuzalisha kakao bora ambayo imekuwa ikitumika kuzalisha bidhaa mbalimbali ikiwamo chokoleti.

Alisema wilaya hiyo inazalisha mazao mengine ya kimkakati ikiwemo michikichi ambayo inatumika kuzalisha mafuta ya mawese pamoja na korosho. Alisema kutokana na upekee wa wilaya hiyo, serikali imewekeza kwenye uboreshaji wa miundombinu ya usafiri na usafirishaji ili kuwarahisishia wananchi kusafirisha mazao yao.

Alisema serikali imejenga Barabara nyingi za lami kwa ajili ya kuunganisha wilaya hiyo na Bandari za Ziwa Nyasa hasa za Itungi na Ngonga zilizopo wilayani humo na Mbamba Bay iliyopo mkoani Ruvuma kisha kuunganishwa na Bahari ya Hindi kwa njia ya Barabara.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera alisema wilaya ya Kyela ni miongoni mwa wilaya nchini ambazo zimenufaika na miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo ya sekta ya kilimo, afya, elimu na miundombinu ya barabara.

Alisema serikali imetoa ruzuku ya miche ya kisasa ya michikichi ambayo inasambazwa kwa wakulima kwa ajili ya kuhamasisha uzalishaji wa zao hilo kwa lengo la kupunguza uagizaji wa mafuta nje ya nchi.

“Lakini kwenye zao la kakao mwaka huu bei imevunja rekodi kwa sababu imepanda kutoka Sh. 2800 ambayo ilikuwepo awali mpaka Sh. 32,000 bei ambayo imetokana na serikali kuimarisha mfumo wa stakabadhi za ghala,” alisema Homera.

Alisema Barabara hiyo ilianza kujengwa na baadhi ya wananchi walibomoa nyumba zao kwa hiyari ili kupisha mradi huo lakini mpaka sasa ujenzi hauendelei na wananchi hawakulipwa fidia.

**“Naomba aina hiyo ya mpunga muitunze ili isipotee kwani ina soko zuri nje ya nchi” Kabudi**

# HALMASHAURI YA MBALIZI
## KUBWA INATULEMEA - VIONGOZI MBEYA DC



*Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Palamagamba John Kabudi akiongea na umati wa watu waliojitokeza kumsikiliza katika kijiji cha Santila kilichopo kata ya Mbalizi.*

Na Lusajo Mwakabuku

Mwenyekiti wa halmashauri ya wilaya ya Mbeya Mhe Mwalingo Kisemba amemuomba Waziri wa Katiba na Sheria Prof. Palamagamba John Kabudi, kuwasaidia kumweleza Rais Samia Suluhu Hassan juu ya ombi lao la kuipandisha hadhi mamlaka ya mji mdogo wa Mbalizi kua halmashauri ya mji ili kuwarahisishia wananchi wa halmashauri hiyo kupata huduma Kwa urahisi na viongozi kuwahudumia wananchi wao Kwa ukaribu.

Mwalingo ameeleza hayo Kwa Waziri Prof. Kabudi akiwa Mbeya ikiwa ni siku ya nne ya ziara yake ya kikazi ya kutembelea halmashauri saba za Mkoa wa Mbeya, Kwa maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan Kwa mawaziri, ambapo amesema halmashauri ya wilaya ya Mbeya imekua kubwa na kuwapa ugumu viongozi kuwahudumia wananchi, hivyo kupandishwa hadhi mamlaka ya mji mdogo wa Mbalizi itakua na msaada mkubwa kwa kusogeza huduma kwa wananchi.

Orani Njeza, Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini alisema kupandishwa hadhi Kwa mamlaka hiyo itakua ni sehemu ya kuligawa jimbo la Mbeya Vijijini pamoja na halmashauri hiyo bila kuanzishwa Kwa eneo jipya la utawala kwakua mamlaka hiyo ya mji mdogo wa Mbalizi tayari Ina viongozi kuanzia ngazi ya watendaji hadi mkurugenzi.

Akijibu maombi hayo Waziri wa Katiba na Sheria Prof. Paramagamba Kabudi, amesema atazungunza na Waziri mwenye dhamana Juu ya kuipandisha hadhi mamlaka hiyo kwakua haikinzani na maelekezo ya Rais ya kuzuia uanzishwaji wa maeneo mapya ya utawala Kwa Sasa.



*Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Palamagamba John Kabudi akikagua mradi wa chanzo cha maji klichopo katika eneo la Forest Jijini Mbeya.*



> “Masoko ina wakazi 5573 kati yao wanawake ni **2962** na wanaume **2611** ambao wataoata huduma za afya kuwa ukaribu zaidi baada ya kituo hicho kukamilika”
>
> *Prof. Kabudi*

### WATOTO WETU WANAJIFUNGUA VICHAKANI - WANANCHI



Waziri wa Katiba na Sheria Prof. Paramagamba Kabudi amemtaka mkurugenzi nakuu wa Wilaya ya Rungwe Mkoani Mbeya kuongeza kasi ya ujenzi wa kituo Cha afya Masoko kinachojengwa kwenye Kijiji Cha Bujesi ili kuharakisha wananchi zaidi ya Elfu Saba kutoka kata za Masoko na Kisiba kupata huduma za Afya Kwa ukaribu.

Prof. Kabudi amesema hayo wakati akiweka jiwe la msingi kwenye kituo Cha afya Cha Masoko kinachojengwa Kwa zaidi ya millioni 500 fedha kutoka serikali kuu, ili kuondoa kero ya kinamama wajawazito kujifungua njiani wakiwa wakati wa kufuata huduma za afya kwa zaidi ya kilomita 20.

Wakizungumza mbele ya Waziri wananchi wa Kijiji Cha Bujesi Kata ya Masoko Wilaya ya Rungwe Mkoani Mbeya wamesema kumekua na shida kubwa ya huduma za afya kwenye Kata yao Hali inayosababisha wajawazito wengi kujifungua njiani kutokana na kufuta huduma hiyo umbali mrefu kutoka Kijiji chao Hadi hospitali ya Wilaya ya Makandana.

Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022 kata ya Masoko ina wakazi 5573 kati yao wanawake ni 2962 na wanaume 2611 ambao wataoata huduma za afya kuwa ukaribu zaidi baada ya kituo hicho kukamilika.

# Samia Anaboresha Mazingira Kwa Watoto Wenye Mahitaji Maalum.

by Lusajo Mwakabuku

Waziri wa Katiba na Sheria Prof. Paramagamba Kabudi amesema serikali ya awamu ya sita inaendelea kuboresha miundombinu ya elimu Kwa watoto wenye mahitaji maalum kwenye shule mbalimbali ili kurahisisha watoto hao kujifunza katika mazingira bora.



Prof. Kabudi ameeleza hayo wakati akiweka jiwe la msingi ujenzi wa bweni la watoto wakike wenye mahitaji maalum kwenye shule ya msingi Sama wilayani Kyela, ikiwa ni muendelezo wa ziara yake ya kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo Mkoani Mbeya Kwa maelekezo ya Rais wa Tanzania Dkt Samia Suluhu Hassan, ambapo ametaka ujenzi huo uzingatie ubora na urafiki Kwa watoto hao hasa kwenye maeneo ya vyoo na bafu kwenye bweni hilo.

“Mimi nimebahatika kusoma shule ambayo ilikuwa ya mchanganyiko na watu wenye mahitaji maalum na ninafahamu kuwa watu hawanapenda sana usafi na ni maelekezo ya Rais Samia kuwa mazingira yawe rafiki na ya kuvutia hivyo nakuagiza wewe mhandisi unayekamilisha kazi hii kuhakikisha hilo limezingatiwa” Alisema Kabudi.

Donisia Kipoti Ni mlezi wa watoto wenye mahitaji maalum kwenye shule ya msingi Sama, anasema mwanzo kabla ya ujenzi wa miundombinu mipya, watoto wenye ulemavu walikua wanakabiliwa na changamoto kubwa ya kujisitili kutokana na miundombinu kuto kua rafiki kwao na kusababisha magonjwa ya Mara Kwa Mara Kwa watoto huku Mwalimu mkuu wa shule hiyo akieleza umuhimu wa shule hiyo Kwa wazazi.

# Matukio katika Picha



*Idadi kubwa ya wananchi wamejitokeza katika ziara ya Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Prof . Palamagamba John Kabudi akiwa ameambatana na na Mkuu wa Mkoa na wataalam mbalimbali kutoka mkoani na taasisi.*



*Mkuu wa Mkoa wa Mbeya Komredi Juma Homera akiwasalimia wananchi na kuonesha furaha yake baada ya muitikio mkubwa.*



*Mkuu wa Mkoa wa Mbeya Komredi Juma Homera akinong'onezana neno na Mwenyekiti wa CCM Mkoani Mbeya.*

*Waziri kabudi akikagua chumba cha upasuaji ambacho kimewekwa vifaa vya kisasa kwa ajili ya huduma mbalimbali za upasuaji*





*Ukaguzi ukiendelea katika kiwanda cha kuzalisha Carbon dioxicide inayotumika katika viwanda mbalimbali vya kutengenezea soda na bia.*

*Baadhi ya wanafunzi wa shule ya sekondari Mwakaleli wakifanya experiment mbele ya Waziri Kabudi baada ya kupata jengo la labaratory.*





*Waziri wa Katiba na Sheria akihutubia wananchi wa Bukokelo wilaya ya Rungwe jijini Mbeya.*